**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari DR. OLSEN**

**S.L.P.134, MBULU**

**Tarehe 26/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI DR.OLSEN HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU MKOA MANYARA MWAKA 2024/2025**

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka **2024/2025** tahasusi ya PCB/CBG. Shule ya sekondari Dr. Olsen ipo kata ya Haydom katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

   Unaweza kufuka Dr. Olsen sekondari kwa kutumia usafiri wa aina mbalimbali kama ifuatavyo;-.

   A. Magari madogo aina ya **land cruiser** kutoka Arusha kupitia Mbulu – Haydom – au
   B. Kutumia usafiri wa basi la **SUNVIC** kutoka Arusha –Karatu- Mbulu hadi Haydom au
   C. Usafiri wa basi la **MTEI na MANYARA LINE** kutokaArusha – Katesh – Haydom au
   D. kutoka Singida – Haydom kwa basi la **JESUS LOVE, Ester coach, Na magari madogo aina ya LAND CRUISER** na mengineyo.
   E. Pia unaweza kusafiri kutoka IGUNGA hadi Haydom kwa usafiri wa basi la **JESUS LOVE**
   F. Pia unaweza kusafiri kutoka DODOMA hadi Haydom kwa kutumia usafiri **ESTER TRANS**
   G. Pia unaweza kusafiri kutoka Mwanza hadi Haydom kwa basi la JESUS LOVE.

Muhula wa Masomo utaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024.

## 1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 1.1 Sare za Shule

(a) Mwanafunzi anatakiwa ajishonee sare za shule kwa kufuata maelekezo ya mashono kama ilivyo kwenye michoro/picha iliyoambatishwa. Pia aina ya kitambaa kimeambatishwa na fomu hii.

(i) Sare ya shule hii ni sketi ndefu rangi ya damu ya mzee (namba moja) na sweta la rangi ya damu ya mzee pea mbili – utajishonea



Rangi ya damu ya mzee

(ii) Shati jeupe ya mikono mirefu pea mbili – utajinunulia

(iii) Tai ndefu ya damu ya mzee yenye michirizi miwili meupe kama inavyoonekana kwenye mchoro/picha – utajishonea

(iv) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na gidamu visivyo na visigino virefu vyenye kufunika mguu wote pea mbili (2) kwa ajili ya darasani.

(v) Soksi jozi nne nyeupe au zaidi kulingana na uwezo .

(vi) Pulneck nyeupe/ rangi ya sketi za kutosha zisizo na mapambo ya aina yoyote.



### (b) SARE ZA SHULE KWA WANAFUNZI WA KIISLAMU

Wasichana wa madhehebu ya kiislamu wanapaswa kuvaa “HIJABU” (kijuba) kulingana na maadili ya dini yao na si vinginevyo.

1. Sketi mbili za rangi ya damu ya mzee – utajishonea kama picha inavyoonyesha

2. Shati mbili nyeupe mikono mirefu na “**HIJABU” NYEUPE ISIYO NA UREMBO WA AINA YOYOTE** – wala maandishi kwa darasani na nyeusi nje ya darasa.
3. Kinyume na maelezo ya mashono hutapokelewa



**(a) Sare ya michezo kwa shule hii ni**

Bukta ya blue inayopita kwenye magoti, raba nyeusi pea moja (1) na
T – Shirt ya shule ya njano yenye maandishi **Dr. Olsen sekondari kwa nyuma na nembo ya shule kifuani upande wa kushoto,** sampuli inapatikana shuleni.

(b) Nguo za kushindia (shamba dress) Sketi mbili za rangi ya kijani kibichi na tisheti ya kijani isiyo na maandishi yoyote kwa ajili ya kazi za nje kama ilivyo kwenye michoro/picha iliyoambatishwa.



**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari matano (5) counter book Q4 kwa kuanzia.
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) na ruled 1 kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);

***Nunua kulingana na uwezo wako sio lazima***.

| S/N | Tahasusi | Jina la kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|---|
| **a.** | Physics | - Principles of physics for class XI | - S. Chand |
| | | - Principles of physics for class XII | - S. Chand |
| | | - Physics for advanced level secondary schools book five | - TIE |
| | | - Physics for advanced level secondary schools book six | - TIE |
| | | - ABC PHYSICS | - SATISH GUPTA<br>- ER. SUNIL BATRA |
| **b.** | Biology | - Understanding biology advanced level | - |
| | | - Biological science third edition | - TAYLAR DJ(1997) |
| | | - Biology for advanced Level Secondary school student's book form five | - TIE |
| | | - Biology for advanced Level Secondary school student's book form six | - TIE |
| | | - S. CHAND'S Biology for class XI 3500 Multiple choice questions | - DR. P. S. VERMA<br>- DR. B. P. PANDEY |
| **c.** | Chemistry | Conceptual chemistry for class XII volume I & II with valuebased questions | S. CHAND<br>DR. S. K. JAIN |
| | | Conceptual chemistry for class XI volume I & II with valuebased questions | S. CHAND<br>DR. S. K. JAIN |
| | | - Inorganic Chemistry for advanced Level Secondary school students book form five and six | - Tanzania Institute of Education |
| | | - Organic Chemistry for advanced Level Secondary school students book form five and six | - Tanzania Institute of Education |
| | | - Physical Chemistry for advanced Level Secondary school students book form five and six | - Tanzania Institute of Education |
| | | - General Chemistry for advanced Level Secondary school students book form five | - Tanzania Institute of Education |
| | | - Advanced level practical chemistry | - MANDIA BOOK SERIES |
| **d.** | Geography | - Physical geography in concise for Advanced Level | - ZUBERI |
| | | - Comprehensive approach to physical geography for Advanced Level | - JAMES EGINO KINUNDA |
| | | - Practical geography in concise for Advanced Level | - ZUBERI |
| | | - Human geography for Advanced Level secondary School Students Book for Five and Six | - TIE |
| | | - Practical geography for Advanced Level secondary School Students Book for Five and Six | - TIE |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | - Physical geography for Advanced Level secondary School Students Book for Five and Six | - TIE |
| **e.** | GENERA L STUDIES | - General studies for Advanced Level Secondary School Students Book Form Five and Six | - TIE |
| **F.** | Basic Applied Mathemati cs | - Basic applied MATHEMATICS for Advanced Level Secondary School Students Book Form Five and Six | - Tanzania Institute of education |

- Mahitaji mengine kwa usalama
  - Mwavuli mmoja, buti ya matope kwa ajili ya shughuli za nje wakati wa mvua.
  - Track suit pea 1 ya rangi ya blue nyeusi (dark blue) yenye mstari mweupe pembeni, kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa kujisomea
  - Sanduku la bati/chuma la kufunga kwa kufuli imara
  - Pazia moja la rangi ya light blue zitapatikana shuleni kwa bei nafuu na kwa utaratibu maalum
  - ***Koti moja la maabara jeupe (white laboratory coat) pamoja na maski kwa ajili ya mazoezi ya sayansi kwa vitend.***

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Non – programmable Calculator;
vi. Godoro moja (1) la futi 2.5 x inch 4 na mto mmoja (1) na foronya mbili za rangi ya blue bahari.
vii. Chandarua ya mbu – mstatili (rangi yoyote), Blanket moja (1) nzito, Taulo moja (1), night dress, shuka ya rangi ya blue bahari pea mbili.
viii. Vifaa vya usafi
- Ufagio mmoja wa kufagia nje na mmoja (1) wa kufagia ndani
- Mopa moja (1) kwa ajili ya usafi wa mazingira
- Shoka 1 lenye uzito wa kuanzia kg3 na lenye mpini imara.
- Panga moja (1) lenye mpini imara.

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) zote za aluminium na zitapatikana kwenye duka la shule
x. Nguo za ndani za kutosha;
xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

### 1.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya shule Benki ya **NMB kwa Ac. 41201200047**, jina la Akaunti ni **Dr. Olsen Sec. School Recurrent Account**.

- **Wanafunzi wanatakiwa kujiunga na mfuko wa bima ya afya NHIF. Uje na Tsh. 50,400/= taslim kama huna bima kwa ajili ya matibabu ili usajiliwe kwenye mfuko wa bima ya afya kwa kipindi cha mwaka mmoja na fedha za bima haziwekwi kwenye akaunti.**

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

  - **Mkuu wa shule 0784909514**
  - **Makamu Mkuu wa Shule 0624030173**
  - **Mwandamizi Taaluma 0744504480**
  - **Mwandamizi Malezi 0786259962**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

3. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

MBULU DISTRICT COUNCIL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**HEADMISTRESS,**
**DR. OLSEN SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 134,**
**DATE 26/04/2024.**

**REF.NO. DR. OSS/JOIN F5/135/VOL.1/16**
**TO MEDICAL OFFICER, ……………………………………………………………**
**FULL NAME**
**…………………………………………………………………………………………**

Please examine the above named pupil as to her fitness for entrance to this school in form V – 2024/2025.

i. Stool Examination…………………………………………………………………………
ii. Blood counter (red and white)……………………………………………………………
iii. Urinal analysis ……………………………………………………………………………
iv. T.B Test …………………………………………………………………………………
v. Syphilis Test………………………………………………………………………………
vi. Eye Test…………………………………………………………………………………
vii. Chest………………………………………………………………………………………
viii. Spleen ……………………………………………………………………………………
ix. Abdomen …………………………………………………………………………………
x. Check cases of pregnancy ………………………………………………………………
xi. Additional information e.g. Physical defect or impairment, infection, chronic family diseases etc.……………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by the medical officer)

I have examined the above and consider that she is physically fit for appointment /engagement as above

Date ……………………………………  Signature ……………………………….

Station ………………………………Designation …………………………

Note to medical officer at the time of examination

“Please treat individual for an ailment you noted.”

**************** **DELETE AS NECESSARY** *********************

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

**A. FOMU NA. 02**

**MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI**

SEHEMU A (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

1. Jina la mwanafunzi (majina matatu)………………………………………………………
2. Uraia………………………………………………………………………………………
3. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………………
4. Shule anakotoka……………………………………………………………………………
5. Tarehe ya kutoka shule hiyo………………………………………………………………

**SEHEMU B: ( Ijazwe na mzazi/mlezi)**

1. Jina la mzazi/mlezi (majina matatu) ……………………………………………………
2. Anwani ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………
3. Mahali anapoishi (Kijiji/Kata)………………………………………………………………
4. Kazi ya mzazi/mlezi…………………………………………………………………………
5. Mahali anapofanya kazi ……………………………………………………………………
6. Ndugu wawili wa karibu (wanaweza kuwa badala ya mzazi/mlezi)

(a) Jina ………………………………………………………………………………

Anwani yake …………………………………………………………………………………

Uhusiano wake na mwanafunzi………….………………………………………………………

Uhusiano wake na mzazi/mlezi…………………………………..………………………

Tarehe…………………………………………… Sahihi ya mzazi………………………………

(b) Jina ……………………………………………………………………………………

Anwani yake ………………………………………………………………………………..

Uhusiano wake na mwanafunzi…………………………………………………………………

Uhusiano wake na mzazi/mlezi………………………………………………..……………

Tarehe………………………………………………Sahihi ya mzazi……………………………

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

**SHULE YA SEKONDARI YA DR OLSEN,**

**S.L.P 134,**

**MBULU – MANYARA.**

**26/04/2024.**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………………**

**YAH: MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE PIA KUSHIRIKIANA NA SHULE KUMLEA MWANAFUNZI**

**(IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWE)**

1. Jina kamili ………………………………………………………..
2. Kazi yake………………………………………………Umri……………………………
3. Anwani ya nyumbani…………………………………………………….………………
4. Kijiji...................................………
   Kata…………….……….…Tarafa…………..…………Wilaya…………………………
   Mkoa………..……….………Uraia…………..………………
5. (a) Dini ya mzazi/Mlezi…………………………..………………………………………
   (b) Namba ya simu kama ipo……………………………Mji……………………………

6. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe…………………………………………………
7. Anwani kamili ya nyumbani ambapo mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo……………………………………………………………………………………………
8. Anwani ya kazini ikiwa inatofautiana na hiyo hapo juu na kila mara inapobadilika tunaomba utuarifu rasmi kwa barua kupitia kwa mkuu wa kituo/Mwenyekiti wa kijiji chako/mwajiri wako……………………………………………………………………
9. Nimesoma barua ya kuripoti shuleni, sheria za shule na fomu zote zilizoambatishwa. Nimeelewa na kuridhika na ninakubali wajibu huo nikijua ni ahadi ambayo sitaweza kukiuka bila kuhitaji hatua za kisheria zinazostahili kuchukuliwa dhidi yangu.
10. Naahidi wakati wote kushirikiana na kusaidiana na waalimu katika kumlea kijana wangu ili awe na tabia njema siku zote, mchapakazi na mwenye bidii ya masomo. Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule. Juu ya hayo naelewa mwanangu akienda kinyume na sheria za shule hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Nathibitisha kwamba habari zilitolewa hapo juu ni kamili na ni za kweli

Jina la mzazi/mlezi………………………….Sahihi…………………Tarehe……………………

Jina la Afisa Mtendaji ……………………Sahihi ya Afisa Mtendaji …………… tarehe ………


iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**A. PICHA (4) ZA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA SHULENI**

| S/N | PICHA | UHUSIANO | NO. YA SIMU |
|---|---|---|---|
| 1. | Bandika picha hapa (passport size) | • BABA MZAZI/MLEZI | |
| 2. | Bandika picha hapa (passport size) | • MAMA MZAZI/ MLEZI | |
| 3. | Bandika picha hapa (passport size)<br><br>Bandika picha hapa (passport size) | • NDUGU WA KARIBU (2) WA MWANAFUNZI WAKAOWEZA KUMTEMBELEA SHULENI (TAJA UHUSIANO)<br>A. …………………………………..<br><br>B. …………………………………. | |

1. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

Kwa niaba ya Jumuiya ya Dr. Olsen sekondari napenda kukukaribisha SANA hapa shuleni, na nakutakia safari njema ya kuja shuleni.




**NAKALA:**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU,**

**S. L. P 74, MBULU – MANYARA.**

**SHULE YA SEKONDARI YA DR OLSEN,**
**S.L.P 134,**
**MBULU – MANYARA.**
**26/04/2024.**

**KWA MWANAFUNZI ……………………………………..**

**YAH: <u>MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI (KUWA MTIIFU NA MWENYE NIDHAMU KWA MUDA WOTE AWAPO SHULENI).</u>**

1. Mimi ……………………………………………………..wa kidato chatano mwaka 2024/2025.Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu,
2. Jina…………………………………………………………………………………………
   (a) Nitatii amri zote za Dr. Olsen Sekondari pamoja na miongozo mbalimbali ambayo imetolewa na viongozi wa shule kuanzia ngazi ya kiongozi wa darasa(monitor), viranja, wafanyakazi wasio waalimu, waalimu na Mkuu wa shule;
   (b) Kuwa nitatimiza wajibu wangu ulionileta hapa shuleni ambao ni kusoma.;
   (c) Kuwa nitahudhuria masomo darasani na mahali pengine popote nitakapohitajika;
   (d) Kuwa nitakuwa ndani ya mipaka ya Dr Olsen Sekondari wakati wote niwapo shuleni ,labda tu kwa shida maalum na baada ya kupata ruhusa ya kutoka nje,kwa mwalimu wa zamu au mwenye dhamana ya ruhusa.
   (e) Naahidi kuwa baada ya kuyaelewa yote hapo juu, nitapokea na kutii maagizo, sheria , amri na maelezo ambayo yatatolewa mara kwa mara shuleni. Sitaenda kinyume na ahadi hii .Nikienda kinyume na sheria za Shule hatua kali zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kufukuzwa shule.
3. Jina ………………………..…Sahihi ya Mwanafunzi………………Tarehe………………
4. Jina la mzazi/mlezi……………………………Sahihi………………Tarehe………………..
5. Jina la Shahidi…………….…………………Sahihi……………..Tarehe…………………….

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Jina la Makamu Mkuu wa Shule**……………………………………………………………..

**Sahihi ya Makamu Mkuu wa Shule**………………………………**Tarehe**……………………